**CHAPISHO LA MAELEZO YA CHANJO** SWAHILI

# Chanjo ya homa ya manjano

## *Kile Unachopaswa Kukijua*

Machapisho Mengi ya Maelezo ya Chanjo yanapatikana katika lugha ya Kihispaniola na lugha nyingine. Tazama www.immunize.org/vis

Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

## 1 Kwa nini upatiwe chanjo?

Homa ya manjano ni ugonjwa hatari unaoathiri ini. Husababishwa na virusi vya homa ya manjano. Homa ya manjano inaweza kusababisha homa kali ambayo hudumu kwa majuma machache, au inaweza kusababisha homa kali ya mara kwa mara.

Maambukizi ya virusi vya homa ya manjano yanaweza kuwa makali au sugu.

**Maambukizi makali ya virusi vya homa ya manjano** ni homa ya muda mfupi ambayo hutokea ndani ya miezi 6 ya mwanzo baada ya mtu kuambukizwa virusi vya homa ya manjano. Hii inaweza kusababisha:

- homa, uchovu, kupoteza hamu ya kula, kichefuchefu na/au kutapika
- homa ya nyongo ya manjano (ngozi au macho ya njano, mkojo mweusi, kinyesi cha rangi ya mfinyanzi)
- maumivu katika misuli, viungo, na tumbo

**Maambukizi sugu ya virusi vya homa ya manjano** ni homa ya muda mrefu ambayo hutokea pindi virusi vya homa ya manjano vinapobakia mwilini mwa mtu. Watu wengi ambao wanaumwa homa ya manjano sugu hawana dalili, lakini bado ni hatari na inaweza kusababisha:

- kuharibika kwa ini (cirrhosis)
- saratani ya ini
- kifo

Mtu mwenye maambukizi sugu ya homa ya manjano anaweza kuwaambukiza wengine, hata kama wenyewe hawajihisi au hawaonyeshi
kuumwa. Hadi watu milioni 1.4 nchini Marekani wanaweza kuwa na maambukizi sugu ya homa ya manjano. Karibia 90% ya watoto wadogo wanaopata homa ya manjano huwa na maambukizi sugu na karibia 1 kati ya watoto 4 hufa.

Homa ya manjano huambukiza pale damu, shahawa, au maji maji mengine ya mwili wana maambukizi ya virusi vya homa ya manjano yanapoingia kwenye mwili wa mtu ambaye hana maambukizi. Mtu anaweza kupata maambukizi ya virusi kupitia:

- Kuzaliwa (mtoto ambaye mama yake ana maambukizi anaweza kuambukizwa wakati au baada ya kuzaliwa)
- Kutumia vitu kama vile nyembe au miswaki pamoja na mtu mwenye maambukizi
- Kugusana na damu au jeraha la mtu mwenye maambukizi
- Kujamiana na mtu mpenzi mwenye maambukizi
- Kutumia sindano, bomba la sindano, au vifaa vingine vya kutundikiwa dawa
- Kutolewa damu kwa kutumia sindano au kifaa chenye ncha kali

Kila mwaka karibia watu 2,000 nchini Marekani hufa kwa homa ya manjano kunakohusiana na magonjwa ya ini.

**Chanjo ya homa ya manjano** inaweza kuzuia homa ya manjano na madhara yake, pamoja na saratani ya ini na maambukizi sugu ya homa ya manjano.

## 2 Chanjo ya homa ya manjano

Chanjo ya homa ya manjano imetengenezwa kutokana na sehemu ya virusi vya homa ya manjano. Haiwezi kusababisha maambukizi ya homa ya manjano. Chanjo mara nyingi hutolewa kudungwa sindano 2, 3, au 4 zaidi ya mwezi 1 hadi 6.

**Watoto wadogo** wanapaswa kupata chanjo ya homa ya manjano wakati wamezaliwa na kwa kawaida hukamilisha dozi wafikapo umri wa miezi 6.

**Watoto wote na vijana** chini ya miaka 19 ambao bado hawajapata chanjo wanapaswa pia kupatiwa chanjo.

Chanjo ya homa ya manjano inapendekezwa kutolewa kwa **watu wazima** ambao hawajachanjwa na wapo hatarini kupata maambukizi ya virusi vya homa ya manjano, ikiwemo:

- Watu wanaojamiana na wenza wao wenye maambukizi ya homa ya manjano
- Watu wenye hisia za ngono ambao hawapo kwenye mahusiano ya mpenzi mmoja kwa muda mrefu
- Watu wanaotaka vipimo au matibabu ya magonjwa ya zinaa
- Wanaume mwenye mahusiano ya kimapenzi na

wanaume wengine

- Watu ambao wanatumia sindano, bomba la sindano, au vifaa vingine vya kutundikiwa dawa pamoja
- Watu katika kaya ambao wanagusana na mtu mwenye maambukizi ya virusi vya homa ya manjano
- Wahudumu wa afya na wafanyakazi wa usalama wa umma wapo hatarini kupata maambukizi kupitia damu na maji maji
- Wakazi na wafanyakazi katika makazi ya watu wenye ulemavu
- Watu katika makazi ya jumuiya
- Waathirika wa shambulio au uzalilishaji wa kingono
- Wasafiri kuelekea mikoa mingine wenye viwango vikubwa vya homa ya manjano
- Watu wenye ugonjwa sugu wa ini, figo, maambukizi ya VVU, au kisukari
- Yeyote anayetaka kujikinga dhidi ya homa ya manjano

Hakuna madhara yanayofahamika ambayo yanasababishwa na chanjo ya homa ya manjano kama ilivyo katika chanjo nyinginezo.

## 3 Kuna baadhi ya watu hawapaswi kupatiwa chanjo

z

Mwambie mtu anayekupatia chanjo hiyo:

- **Ikiwa mtu anayepatiwa chanjo ana tatizo la mzio linalohatalisha maisha yake.** Ikiwa hukuwahi kuwa na mzio unaohatarisha maisha baada ya dozi ya chanjo ya homa ya manjano, au una mzio mkali katika sehemu yoyote ya ya chanjo hii, unaweza kushauriwa kutopatiwa chanjo. Muulize mtoa huduma za afya wako ikiwa unahitaji taarifa kuhusu vipengele vya chanjo.
- **Ikiwa mtu anayepatiwa kinga hajisiki vizuri.** Ikiwa una homa kali, kama vile baridi, kuna uwezekana wa kupata chanjo leo. Ikiwa unaumwa kidogo au sana, unaweza kusubiri hadi upate nafuu. Daktari wako anaweza kukushauri.

## 4 Hatari ya matokeo ya chanjo

Dawa yoyote, ikiwemo chanjo, kuna uwezekano wa uwepo madhara. Madhara haya mara nyingi ni madogo na huisha yenyewe, lakini madhara makubwa pia yanaweza kutokea.

Watu wengi wanaopata chanjo ya manjano hawajasababishiwa matatizo yoyote na chanjo hiyo.

**Matatizo madogo** yanayoweza kusababishwa na chanjo ya homa ya manjano ni pamoja na:

- kuwasha sehemu ilipodungwa sindano ya chanjo
- joto la 99.9°F au zaidi

Ikiwa matatizo haya yanatokea, mara nyingi huanza punde baada ya kudungwa sindano na kudumu kwa siku 1 au 2.

Daktari wako atakushauri zaidi kuhusu matokeo haya.

**Madhara mengine yanayoweza kutokea baada ya chanjo hii:**

- Watu wakati mwingine huzirai baada ya taratibu za matibabu, ikiwamo kupatiwa chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takribani dakika 15 kunaweza kukusaidia kukukinga dhidi ya kuzirai na majeraha yasababishwayo na kuanguka. Mueleze muhudumu wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au una mabadiliko ya uoni au kusikia kengele masikioni.
- Baadhi ya watu hupata maumivu ya bega ambayo yanaweza kuwa makali na kudumu muda mrefu kuliko muwasho wa kawaida unaweza kutokea baada ya kudungwa sindano. Hili hutokea mara chache sana.
- Dawa yoyote inaweza kusababisha madhara makubwa ya mzio. Madhara kama hayo yanayoweza kusababishwa na chanjo ni mara chache sana karibia chanjo 1 ya milioni, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi masaa machache baada ya kupata chanjo.

Kama ilivyo katika dawa nyingine yoyote, kuna uwezekano wa mbali wa chanjo kusababisha majeraha makubwa au kifo.

Usalama wa chanjo mara zote huwa chini ya uangalizi. Kwa taarifa zaidi, vinjari: **www.cdc.gov/usalamawachanjo/**

## 5 Je, itakuwaje ikiwa kuna tatizo kubwa?

### Je, nini ninapaswa kuangalia?

- Angalia chochote ambacho kinakuhusu, kama vile ishara vya matatizo makubwa ya mzio, homa kali, au tabia isiyo ya kawaida.

  Ishara ya **matatizo makali ya mzio** yanaweza kujumuisha mabaka kwenye ngozi, uvimbe wa uso na koo, kupumua kwa tabu, mapigo ya moyo kwenda mbio, kizunguzungu, na kudhoofu. Haya yanaweza kuanza dakika chache hadi masaa machache baada ya chanjo.

**Je, nini ninapaswa kufanya?**

- Ikiwa unadhani ni **matatizo makali ya mzio** au dharura nyingine ambayo haihitaji kusubiri, piga simu 9-1-1 au nenda hospitali iliyo karibu yako. Vinginevyo, wapigie kliniki yako.

  Halafu, matatizo yaripotiwe katika Mfumo wa Matukio Yasiyofaa ya Chanjo (VAERS). Daktari wako anaweza kufungua shauri hilo, au unaweza kufungua wewe mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS **www.vaers.hhs.gov**, au kwa kupiga simu **1-800-822-7967**.

*VAERS haitoi ushauri wa matibabu.*

## 6 Mpango wa Kitaifa wa Fidia ya Majeraha ya Chanjo

Mpango wa Kitaifa wa Fidia ya Majeraha ya Chanjo (VICP) ni mpango wa serikali ambao ulianzishwa kufidia watu ambao wanaweza kuwa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu ambao wanaamini kwamba wamesababishiwa majeraha na chanjo wanaweza kujifunza kuhusu mpango huu na kuhusu kuanzisha malalamiko kwa kupiga simu 1-800-338-2382 au kuvinjari tovuti ya VICP www.hrsa.gov/fidiayachanjo. Kuna ukomo wa muda kufungua malalamiko ya fidia.

## 7 Je, nawezaje kujua zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya. Yeye anaweza kukupatia bunda la chanjo au anaweza kukuelekeza vyanzo vingine vya taarifa.
- Wapigie idara ya afya ya kijiji au nchi.
- Wasiliana na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC):
  - Piga**1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  -Vinjari tovuti ya CDC **www.cdc.gov/vaccines**

Vaccine Information Statement
Hepatitis B Vaccine
Kiswahili (Swahili)

Office use only

10/12/2018 | 42 U.S.C. § 300aa-26

Kuwawezesha wahudumu wa afya kupata habari sahihi juu ya kinga maradhi, upimaji wa kinga maradhi, na ratiba liyopendekezwa ya utoaji wa kinga maradhi hapo mbeleni, habari zitatumwa kwenye kituo cha Usajili wa uboreshaji huduma za Matibabu cha Michigan (Michigani Care Improvement Registry). Watu binafsi wana haki ya kuomba kwamba mhudumu wao wa afya asitume habari zinazohusu kinga maradhi kwenye kituo cha usajili.

DCH-0450SW
AUTH: P. H. S., Act 42, Sect. 2126.
Translation provided by St. Peter's Health Partners, Albany, NY